# Watano wafariki kwa ajali ya moto Dar

**NA MUSSA KHALID, DAR ES SALAAM**

WATU watano wa familia moja wakazi wa Kata ya Pugu Stesheni Manispaa ya Ilala jijini Dar es salaam wamefariki dunia usiku wa kuamkia jana kwa ajali ya moto.

Imeelezwa ajali hiyo ambayo ilitokea katika nyumba ya Edward Jeremia Katemi ambaye ndiye baba wa familia hiyo imesababishwa na hitilafu za umeme majira ya saa nne za usiku.

Akifanya mahojiano na Gazeti hili katika eneo la tukio jana jijini Dar es salaam Edward Katemi amesema waliofariki katika ajali hiyo ni pamoja na Mke wake Jackline Frenk, Mdogo wake Ester Katemi na watoto wake watatu Edwin Katemi Edson Katemi pamoja na Evon Katemi.

Katemi alisema umeme ulikuwa umekatika tangu majira ya asubuhi hivyo ulivyorudi ukazima kisha ukarudi ukawaka tena akashangaa mita ikaanza kuwaka na hivyo kusababisha moto kuwaka eneo zima la nyumba.

"Wakati narudi nyumbani kutoka kwenye mihangaiko yangu nilikuta umeme mara ndio unarudi nikaona kwenye chumba cha ukutani kunapiga cheche ndipo umeme ukalipuka hivyo tukatoka pamoja kwa na majirani kufanya jitihada za kuzima lakini ikashindikana," alisema Katemi.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Pugu stesheni Shukuru Mohamedi Mwinjuma alisema alipokea taarifa majira ya saa sita usiku kutoka kwa mwananchi wake kuwa nyumba hiyo imepata hitilafu ya umeme na kuanza kulipuka.

Mwinjuma alisema mwananchi alimuambia walianza kuvunja nyumba hiyo na kutoa miili hiyo kisha kuwapeleka hospitali ya Nguvukazi Chanika.

Kamanda Maalum wa Jeshi la Polisi ACP Janet Magomi akithibitisha kutokea kwa tukio hilo amebainisha alisema familia hiyo ya watu watano wamefariki kwa ajali hiyo ya moto.

"Baada ya kuchukua miili hiyo tumewakuta watu hawajaungua hamna mahali wamepata majeraha mazingira yaliyoonekana moshi na tuliwachukua na kuwapeleka Hospitali Chanika hivyo upelelezi unaendelea kujua hasa chanzo chake na habari hizo ni za ukweli kabisa," alisema ACP Magomi.

Katika Hatua nyingine ACP Magomi aliwataka wananchi kuwa makini katika kipindi cha mvua hasa wanaoishi mabondeni kuchukua tahadhari ili kuepukana na madhara yanayoweza kujitokeza yanayosababishwa na mvua.

# Wawili kizimbani kwa kuisababishia TCRA hasara ya Mil. 267.6



*Wananchi wakipata maelezo ya ufugaji bora wa samaki kutoka kwa Afisa Uvuvi Mwandamizi, Nelson Mbawala wakati wakitembelea mabanda ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwenye maonyesho ya Maadhimisho ya Siku ya Chakula Duniani yanayoendelea kwenye Viwanja vya Mjimwema kitaifa mkoani Njombe Oktoba 10-16, 2020*

**NA MWANDISHI WETU, DAR ES SALAAM**

WAKAZI wawili wa jijini Dar es Salaam, wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu wakikabiliwa na mashtaka manne likiwemo la kuisababishia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) hasara ya Sh milioni 267.6.

Katika hati ya mashtaka iliyosomwa mahakamani hapo na wakili wa serikali Mwandamizi Wankyo Simon akisaidiana na wakili wa Serikali Jackline Nyantori na Yusuph Abood imewataja washtakiwa hao kuwa ni Baraka Mtunga (41) a mhandisi na mkazi wa Mikocheni na Mfanyabiashara Rajabu Katunda (42) anayeishi Kinondoni.

Mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Kassian Matembele imedaiwa kati ya Desemba 13, 2019 na Septemba 28 mwaka huu katika maeneo ya Hifadhi ya Taifa ya Saadani katika kijiji cha Kajunjo wilayani Bagamoyo mkoani Pwani na maeneo ya jiji la Dar es Salaam washtakiwa kwa pamoja waliongoza genge la uhalifu kwa lengo la kujipatia faida.

Ikiendelea kudaiwa kuwa siku na mahali hapo hapo washtakiwa hao waliimiliki na kutumia vifaa vya mawasiliano vya kielektroniki bila kuwa na leseni ya TCRA huku pia wakidaiwa kutumia vifaa vya kielektroniki kusambaza mtandao wa intaneti bila kuwa na leseni.

Aidha katika shtaka la nne lililosomwa na wakili Nyantori imedaiwa washtakiwa wakiwa na nia ya kukwepa kulipa malipo halali ya mtandao, walisambaza huduma ya mtandao (WiFi) isivyo halali na kusababishia kwa TCRA hasara ya Sh 267,656,794.30.

Katika shtaka la sita inadaiwa washtakiwa hao kwa pamoja walijihusisha na miamala hiyo ya kifedha huku wakijua fedha hizo ni zao la makosa ya kutumia vifaa vya mawasiliano kwa ulaghai na uhalifu wa kupangwa.

Hata hivyo washtakiwa hawakuruhusiwa kujibu kitu chochote mahakamani hapo kwa kuwa mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi za uhujumu uchumi ambazo kwa kawaida kusikilizwa Mahakama Kuu.

Kwa mujibu wa upande wa mashtaka upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika hivyo waliomba tarehe nyingine kwa ajili ya kutajwa na kesi hiyo imeahirishwa hadi Oktoba 27 mwaka huu. na washtakiwa wamerudishwa rumande kwa sababu mashtaka yanayowakabili hayana dhamana kisheria.

Tanzanite gazeti hutolewa na CZ Information & Media Consultant Ltd, Dar es Salaam
Barua pepe: chumbachahabari2020@gmail.com

CHUMBA CHA HABARI

Mwenyekiti wa Bodi +255 757 900 009
Mhariri Mkuu +255 737 900 009
Meneja Masoko/mauzo +255 654 831 113
Usambazaji

Mawakala wa mikoani watume pesa za mauzo kwa namba hii 0654 831113. Benki jina la akaunti ni CZ Information & Media Consultant Ltd.
NMB Benki: 20110026411

Scanned with CamScanner

JAMII NA AFYA

MTANZANIA ALHAMISI OKTOBA 15, 2020

## UGONJWA WA KICHAA CHA MBWA UNAVYOUA

Watu 70, 000 hufariki kila mwaka duniani, huku 1500 hufariki kila mwaka nchini



miaka 15↓

Ndilo kundi linaloshambuliwa zaidi



65%

Kiwango cha mbwa waliopata chanjo lengo likiwa ni 70% ifikapo 2030





96%

Kiwango cha matukio ya kichaa cha mbwa kwa mabara ya Asia na Afrika



Iwapo utang'atwa na mbwa unashauriwa kufanya yafuatayo

Safisha majeraha kwa sabuni au spiriti na maji tiririka kwa dakika 15



Wahi kituo cha Afya kilicho karibu kwa matibabu zaidi



Chanzo: Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto/WHO

Usanifu: Aveline Kitomary

# KICHAA CHA MBWA HAKIAMBUKIZWI KWA KULA NYAMA YAKE - DAKTARI

Uk. iv

Follow us, Like and Subscribe

Mwananchi uk.13&14 Tarehe 15/10/2020

**Ruvuma yaweka mkakati kulifanya Mbambabay kitovu cha utalii**
UK 14

**Unicef yaomba Sh23 kuhudumia wakimbizi nchini**
UK 16

MWANANCHI.CO.TZ
ALHAMISI, OKTOBA 15, 2020
MWANANCHI

# Uchumi



**SIRI YA UMAARUFU WA VITUMBUA BARABARA YA TISA DODOMA** UK 16 - 17 >



Ujasiriamali

# Kutana na Ester katika simulizi ya ufugaji uliompa ubilionea

**Nasra Abdallah**, Mwananchi
nabdallah@mwananchi.co.tz

Safari ya kuutafuta uhuru wa kiuchumi kwa Ester Ng'amilo (53), mkazi wa Tegeta Salasala jijini Dar es Salaam haikuwa lelemama. Amepanda akashuka milima na mabonde.

Akianza na mtaji wa Sh300,000, mama huyu alilazimika kuacha kazi aliyoitumikia kwa miaka saba na kujikita kwenye ufugaji kuku ambao kwa sasa sio tu umebadili maisha yake bali ya familia za watu 25 aliowaajiri wakiwamo watunza bustani, kuku na wanaotengeneza keki.

Ester, mama wa watoto wawili, amedumu kwenye ufugaji kwa zaidi ya miaka 25 sasa baada ya kuachana na mwajiri wake, Shirika la Elimu Kibaha.

Dhamira ya kujikita kwenye ujasiriamali ilitokana na usumbufu aliokuwa akiupata muda mfupi baada ya kuolewa mwaka 1990. Yeye na mumewe walikuwa wanaishi Dar es Salaam hivyo akawa analazimika kwenda Kibaha kila siku. Kutokana na ugumu wa usafiri kipindi hicho, akaacha kazi.

"Nilikaa nikafikiria adha ya kila siku kupanda daladala kwenda na kurudi Kibaha, kipindi hicho na usafiri ulikuwa ni wa tabu, nikaamua kujiajiri katika ufugaji," anasema Ester.

**Alivyoanza ufugaji**

Hata akiwa bado kazini, Ester anasema alikuwa anafuga kuku nyumbani kwake, maeneo ya Kijitonyama walikopanga.

Kipindi hicho anasema alikuwa akifuga kati ya kuku 500 hadi 1,000 wa nyama. Mambo yalibadilika kuanzia mwaka 2000 jirani yake alipomweleza kuhusu kuwapo kwa eneo linalouzwa Salasala.

"Kwa kuwa nilikuwa nina hamu ya kuongeza kuku, nilienda kuona na niliridhika napo. Nilinunua eneo hilo la ekari nne kwa awamu tano. Nimejenga nyumba ya kuishi, kuweka mifugo na nalima," anasema.

Wakati anahamia huko, anasema alikuwa na kuku 1,000 ila sasa wamefika 16,000 wote wakiwa wa mayai kwani kutokana na kuyumba kwa soko wakati wa corona, aliachana na wale wa nyama.

Kwa kuku alionao, kwa siku anasema huwa anaokota zaidi ya trei 250. Kabla hajaachana nao, anasema kwa wiki alikuwa anauza kuku 5,000 wa nyama lakini kufungwa kwa hoteli kipindi cha corona kuliondoa wateja wake muhimu. "Kumkuza kuku mmoja wa nyama mpaka anafika muda wa kufaa kuuzwa ni Sh4,500 wakati wa mayai anagharamu Sh17,000," anasema.

Ingawa alianza kwa Sh300,000 zilizotokana na akiba yake, anasema kuna mambo mengi yametokea ndani ya miaka 25 ya ufugaji wake yaliyochangia kukuza mtaji ambao sasa ni zaidi ya Sh1 bilioni.

Hapa anaitaja Benki ya Akiba (ACB) kuwa mkombozi wake kwani imemlea tangu mwaka 1992 alipokuwa anaanza mpaka sasa. "Nilianza kukopa Sh500,000. Nikihitaji mkopo, naupata ndani ya wiki moja hivyo kuniwezesha kufanya shughuli zangu kwa wakati," anasema.

Ofisa mikopo wa Benki ya ACB, Melchisedec Muhesi anasema ukiachilia mbali uaminifu alinao, Ester ni mfanyabiashara anayetunza kumbukumbu zake kimaandishi jambo linalowarahisishia kujua mahitaji yake.

**INAENDELEA UK 14**

**25**
Miaka ambayo Ester Ng'amilo amejikita kwenye ufugaji kuku.

"Kumkuza kuku mmoja wa nyama mpaka anafika muda wa kufaa kuuzwa ni Sh4,500 wakati wa mayai anagharamu Sh17,000."
Ester Ng'amilo, mfugaji kuku jijini Dar es Salaam.

Scanned with CamScanner

# Lipumba aahidi teknolojia ya uvuvi Mtera

Janeth Joseph, Mwananchi
joseph@mwananchi.co.tz

Isimani. Mgombea urais wa Chama cha Wananchi (CUF), Profesa Ibrahim Lipumba amesema akichaguliwa, atapenyeza teknolojia mpya ya ufugaji na uvunaji samaki katika Bwawa la Mtera lililopo mkoani Iringa.

Teknolojia hiyo amesema itasaidia kupunguza ukosefu wa ajira hasa kwa vijana nchini. Sambamba na hilo, ameahidi kutoa mtaji wa ufugaji samaki ili kuongeza uzalishaji na tija.

Aliyasema hayo katika mkutano wa hadhara uliofanyika Migoli, Jimbo la Isimani alikokuwa akiomba kura jana.

"Najua hapa Iringa kuna wavuvi wa samaki katika Bwawa la Mtera lakini wengi wao wameshindwa kuendelea na shughuli za uvuvi kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo ya kukamatwa na ushuru mkubwa. Tunahitaji kulinda mazingira yenu ili haki ziweze kutendeka. tupeni kura zenu wavuvi muweze kupumua na kuwapunguzia ushuru na shughuli zenu ziweze kuendelea katika hali nzuri," alisema Profesa Lipumba.

"Najua vijana wengi hamna ajira, niwahakikishie wavuvi wote hapa Mtera, ipo teknolojia nzuri ya kufuga samaki hasa kwenye mabwawa makubwa kama hili la Mtera, tunaomba kura zenu ili tuweze kuwapenyezea teknolojia hiyo mpya ya ufugaji samaki, tuwape mtaji wa kufuga samaki muweze kuongeza uzalishaji na mpate kipato kizuri cha kukidhi mahitaji yenu," alisema.

Mgombea huyo alisema samaki wana soko kubwa duniani na nchini na mahitaji yao ni makubwa, vijana wakiwezeshwa kuwafuga kwa wingi kwa teknolojia ya kisasa, tatizo la ajira litapungua kwa kiwango kikubwa katika maeneo yenye mito mikubwa na mabwawa.

"Tupeni kura zenu tukayasimamie mambo haya tuwape vijana wetu uwezo wa kutumia teknolojia bora kuzalisha samaki kwa wingi. Tanzania inakabiliwa na changamoto kubwa ya ajira kwa vijana na hii ni moja ya suluhisho," alisema Profesa Lipumba.

Gazeti hili lilizungumza na baadhi ya vijana waliohudhuria mkutano huo ambao walieleza changamoto wanazokabiliana nazo ukiwamo ukosefu wa ajira.

"Vijana wengi hapa hatuna ajira, maisha yetu magumu sana na wapo wengine walimaliza mpaka vyuo vikuu tunao hapa lakini hawana ajira. Ahadi kama hizi kama kweli zikitekelezwa, basi itakuwa mkombozi kwetu," alisema Mussa Rajabu mkazi wa Migoli.

Alisema ahadi za mgombea wa CUF zinafariji na kuonyesha mwanga kwa sababu vijana wengi wa eneo hilo ni wavuvi, wakiwezeshwa kuwa na mabwawa ya kufugia yatawainua kiuchumi hivyo kuondokana na utegemezi kwa ndugu au marafiki hivyo kushiriki katika maendeleo ya Taifa lao.

Naye mgombea ubunge wa chama hicho Isimani, Nasma Upetu aliwaomba wananchi wa jimbo hilo kumchagua ili akawasilishe kero zao na kusimamia utatuzi wake kwa manufaa ya wananchi wote.

"Najua mkutano wa leo sio wangu lakini wananchi wa Isimani msifanye makosa, nichagueni mimi Oktoba 28 nikawasilishe kero zenu. Nitumeni nikawatumikie na mpigieni kura nyingi Profesa Lipumba kwa sababu ana ndoto kubwa ya kuwatumikia kwa dhati," alisema Nasma.

## SEKTA MUHIMU NCHINI



Tanzania ina rasilimali nyingi za mifugo na uvuvi lakini mchango wake ni mdogo katika uchumi wa Taifa. Mwaka 2018/19, taarifa zinaonyesha sekta ya mifugo ilichangia asilimia 7.6 wakati uvuvi ilikuwa asilimia 1.7. Sababu za mchango mdogo ni uwekezaji mdogo wa sekta binafsi, uzalishaji duni viwandani na ukosefu wa mtaji na mazingira magumu ya kufanya biashara.

Kwa mwaka, Tanzania inatumia Sh100 bilioni kuagiza samaki, maziwa na nyama kutoka nje ya nchi na inatumia Sh251 bilioni kuagiza chakula cha mifugo na samaki. Iwapo bidhaa hizi zingezalishwa nchini, inaaminika zingeleta ajira, kuongeza mapato na kukuza uchumi wa nchi.



Mgombea urais kwa tiketi ya CUF, Profesa Ibrahim Lipumba akizungumza na wanachama na wafuasi wa chama hicho wakati wa mkutano wake wa kampeni uliofanyika katika viwanja vya Chanika, Handeni Mjini mkoani Tanga juzi. Picha na Janeth Joseph

Scanned with CamScanner

# Lissu aahidi kuunda tume ya kuchunguza kero za wavuvi

**Na Waandishi Wetu**

MGOMBEA urais (CHADEMA) Tundu Lissi, jana alilazimika kutumia usafiri wa boti kwenda visiwa vya Ukerewe kuwafikia wapigakura baada ya kukosa kivuko ambacho ilidaiwa kiko kwenye matengenezo.

Katika kampeni zake, Lissu alisema akiingia madarakani, jambo la kwanza ataunda Tume ya Majaji wa Mahakama za Juu kuchunguza matukio yote ya kumiza watu, kuteka watu, kutia umaskini ambayo yamefanyika kwenye mwambao wa Ziwa Nyasa, Ziwa Tanganyika na Ziwa Victoria, ili kufahamu nani aliamuru hayo kutokea, aliyetekeleza na kuchukua hatua kwa mujibu wa sheria za nchi.

"Hakuna sheria ya nchi inayosema ukikuta mtu Ziwa Tanganyia au Victoria adhabu yake kifo, mimi sijaona sheria ya namna hiyo, tutachunguza matukio yote ya mauaji ili tufahamu nani aliyeamuru, aliyetekeleza na nani ashughulikiwe," alisema.

"Kwa sababu kuua ni kosa, lazima wote walioathirika waliouliwa ndugu zao wafidiwe, walioumizwa wafidiwe, waliotiwa umaskini wafidiwe," alisema.

Alisema jambo la pili litakalofanywa ni kubadili sheria na kanuni za uvuvi ili kuhakikisha mambo mabaya hayatokei kwa makundi hayo.

Lissu alisema jingine atakaloshughulikia ni miundombinu karibu na Kisorya ambako kuna umbali mdogo na Kisiwa cha Ukerewe chenye watu zaidi ya 300,000, akiahidi atajenga daraja ili wapate usafiri wa uhakika.

Alisema alilazimika kutumia usafiri wa boti baada ya mara kadhaa kuambia kivuko hicho ni kibovu jambo ambalo kwake aliona ni mbinu kumzuia kuwafikia wananchi wa eneo hilo.

Akizungumza akiwa ndani ya boti hiyo, Lissu alisema zaidi ya mara mbili amefika eneo la Kisorya ili kuvuka lakini alishindwa kwa sababu zilizotolewa na wasimamizi wa kivuko hicho.

"Nimepanda boti baada ya kukosa Kivuko cha kupanda, nilikuja wiki mbili zilizopita kwa ajili ya kampeni, lakini nilishindwa kupanda, yote hii ni kutuzuia tusivuke, lakini tumetumia usafiri mwingine na tumevuka salama, haya yote tumeona ni namna ya kutuzuia kupanda usafiri huo kuwafikia wananchi wa Ukerewe kwa ajili ya kuwafikishia taarifa.

"Kwetu ni Singida, hatuna ziwa, sijawahi kuogelea, lakini nikawaambia watu wangu kama ni kuogelea nitajifunza leo, lakini niende Ukerewe nikazungumze na wana Ukerewe, ninasikia polisi walitaka kuzuia huu mkutano, hawaruhusiwi kuzuia zaidi ya kulinda usalama. Nilisema hata wanizuie lazima nije hapa.

"Poleni sana kwa haya, msivunjike moyo yana mwisho haya na mwisho wake ni Oktoba 28 mwaka huu. Ninawashukuru kwa kuwa sehemu ya kitovu cha mabadiliko ya nchi hasa Kanda ya Ziwa," alisema.

Kwa mujibu wa Lissu, namna ya kumwenzi Baba wa Taifa siyo kuruhusu wanaomheshimu kutoa heshima alikolala, bali kuyaishi mawazo na fikra zake ambazo wengi wameshindwa kuyaenzi. Mgombea huyo alisema Ilani ya CHADEMA inazungumzia uhuru, haki na maendeleo ya watu na kwamba mwaka 1968 aliandika kitabu na kukiita 'Uhuru na Maendeleo', ambacho alisema maendeleo maana yake ni maendeleo ya watu na siyo vitu. Alisema wananchi wa kisiwa na maeneo hayo ni wavuvi, lakini hali zao ni mbaya kwa kuwa kuna waliopoteza maisha, kuchomewa nyavu na mitumbwi na wengine wameishia kwenye umaskini mkubwa. "Ninasema mkinichagua Oktoba 28 mwaka huu, haya mambo ya kunyanyasa wavuvi, kuwatia umaskini itakuwa ni mwisho," aliahidi.

Scanned with CamScanner

Tarehe 14/10/2020

# Lissu: Tutatunga sheria wafugaji kulisha mifugo katika hifadhi

**Peter Elias**, Mwananchi
pelias@mwananchi.co.tz

**Dar es Salaam.** Mgombea wa Chadema wa urais, Tundu Lissu amesema akiwa Rais atatunga sheria itakayowaruhusu wafugaji kulisha mifugo kwenye hifadhi kama walivyokuwa wakifanya kabla ya kutangazwa kuwa za Taifa.

Pia, mgombea huyo amerudia hoja zake kuhusu kufuta vitambulisho vya wafanyabiashara wadogo vinavyotolewa kwa Sh20,000, kuanzisha bima ya afya kwa wote, kupunguza kodi kwa wachimbaji, kuboresha mapato ya wakulima, huku akisisitiza mambo matatu ya ilani ya chama hicho; uhuru, haki na maendeleo ya watu.

Lissu alisema hayo jana katika mikutano yake ya kampeni iliyofanyika Bulyankulu wilayani Kahama, na pia wilaya za Mbogwe na Bukombe mkoani Geita, maeneo ambayo shughuli za kuchumi ni pamoja na kilimo, ufugaji, uvuvi na uchimbaji madini, huku yakiwa karibu na hifadhi.

Alisema kabla kutangazwa kuwa hifadhi za Taifa, wafugaji walikuwapo na walikuwa wakiishi vizuri na wanyamapori bila kuathiri mazingira kama inavyodaiwa.

"Tarehe 29 itakayofuata (siku moja baada ya kupiga kura) hakuna mtu atakamatiwa mifugo yake tena kwa sababu nitapitisha sheria itakayoruhusu wafugaji kuchunga katika maeneo ya hifadhi kama ambavyo walikuwa wakichunga kabla ya hifadhi hazijatangazwa," alisema Lissu huku akishangiliwa.

Mbunge huyo wa zamani wa Singida Mashariki alisema wafugaji wa Mbogwe na maeneo mengine ya jirani wamekuwa wakinyang'anywa mifugo yao kwa kisingizio cha kulisha katika hifadhi za Taifa.

Lissu pia alisema atapunguza utitiri wa kodi kwa wachimbaji wadogo, kuboresha hali za wafanyakazi na kurekebisha uchakatuaji wa mafao yao, akiahidi kutenda haki kwa kila mwananchi ili afurahie maisha.

"Tupeni Serikali, tutaondoa huu utitiri wote wa kodi mnazolipa, tunataka wachimbaji wadogo mnufaike na madini yenu," alisema Lissu wakati akizungumza na wananchi wa Kata ya Bulyankulu wilayani Kahama.

Kuhusu vitambulisho vya wafanyabiashara wadogo, Lissu alisema alirudia kauli yake kuwa atavifuta na atawataka waliokusanya fedha hizo kuzirudisha kwa wananchi.

"Hivi vitambulisho vya wafanyabiashara ni wizi mtupu. Hatuwezi kuacha viendelee kutolewa, tutavifuta na kuwalazimisha wanaokusanya hizo fedha kuzirudisha," alisema Lissu.

Alisema wachimbaji wadogo wamekuwa wakitozwa kodi kwa kila hatua wanayofanya kuanzia kuingia shimoni mpaka hatua ya kuuza madini yao.

Akizungumzia suala ya kodi, mchimbaji mdogo wa Bulyankulu, Mashaka Masalu alikiri kwamba kuna kodi nyingi ambazo wanatozwa ikiwemo kitambulisho cha mfanyabiashara.

"Tumeambiwa ukitaka kuchimba madini lazima uwe na kitambulisho, kwa hiyo tumelipia Sh20,000 kupata kitambulisho. Ukipeleka mchanga kwenye karasha kuna tozo yake, ukitaka kuuza madini yako pia kuna kodi lazima ulipe," alisema.

**NUKUU**

**"Tutapeleka muswada bungeni kuruhusu wafugaji kulisha kwenye hifadhi, sio dhambi."**

Tundu Lissu



**Mgombea urais kwa tiketi ya Chadema, Tundu Lissu akipungia mkono wananchi wa Bukombe walipohudhuria mkutano wake wa kampeni mkoani Geita, Jana. Na**

Scanned with CamScanner

# TDB pondering next step as school milk programme is whittled down






Scanned with CamScanner

Majira Uk.11 Tarehe 14/10/2020

Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi), Dkt. Rashid Tamatamah (kulia) akifafanua jambo kwenye banda la Wizara ya Mifugo na Uvuvi baada ya Mgeni rasmi kwenye uzinduzi wa Maadhimisho ya Kitaifa ya Siku ya Chakula Duniani ambaye pia Naibu Waziri wa Kilimo, Omary Mgumba (kushoto) kutembelea banda hilo mwishoni mwa wiki mkoani Njombe. (Na Mpigapicha Wetu)



Scanned with CamScanner

Nipashe Uk.10 Tarehe 14/10/2020

goza genge la uhalifu, ufujaji na uba-

huku kesi hiyo ikipangwa kutajwa tena Oktoba 26, 2020.



Ofisa Uvuvi Mwandamizi Nelson Mbawala (kushoto), akitoa maelezo ya jinsi ufugaji bora wa samaki unavyofanyika, kwenye mabanda ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, katika maonyesho ya maadhimisho ya Siku ya Chakula Duniani kitaifa, yanayoendelea kwenye viwanja vya Mjimwema mkoani Njombe. **MPIGAPICHA WETU**

Scanned with CamScanner